BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

**BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA PILI**

**Kikao cha Sita – Tarehe 18 Februari, 2026.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Itasomwa.

## I. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

242. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Kumekuwa na malalamiko kwa baadhi ya wananchi kuwa kazi za kusimamia usalama barabarani ambazo kwa mujibu wa Sheria ya Polisi na Askari Wasaidizi, Sura ya 322, Sheria ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, kazi hizo zinatakiwa kufanywa na askari wa jeshi la Polisi ambao wana mafunzo na weledi wa namna ya kufanya kazi hiyo. Hata hivyo, kwa hapa Zanzibar hivi sasa hali imekuwa tofauti na maelekezo ya Sheria kwa kuwa wapo watendaji wa Idara Maalum za SMZ wanafanya kazi hizo tofauti na Sheria inavyoekeleza na wakiwa hawana weledi wala ujuzi wa kufanya kazi hizo.

(a) Sheria gani inawaruhusu watendaji wa Idara Maalum kufanya kazi za usalama barabarani kwa hapa Zanzibar.

(b) Kama ipo sheria hiyo hapa Zanzibar je, hatuoni kwamba inakiuka sheria iliyotungwa na Bunge ambayo inawapa uwezo huo askari polisi peke yake.

(c) Je, Serikali itakuwa tayari kulipa fidia kwa wananchi ambao watapata athari yoyote kutoka kwa watendaji hao pale wanapowakamata na kuchukuwa vyombo vyao na kuwapotezea muda wao, wakati kisheria hawatakiwi kufanya hivyo.

**<u>Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:</u>**

243. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Mnamo mwaka 2000 Mahakama ya Rufaa ya Tanzania ilitoa uamuzi kuwa kosa la uhaini haliwezi kufanyika Zanzibar. Hata hivyo, bado kosa hilo linaonekana lipo katika Sheria ya Adhabu ya mwaka 2018.

Je, kwanini bado kosa hilo limewekwa kwenye sheria wakati Mahakama ya Rufaa ilishatoa uamuzi kuwa haliwezi kufanyika Zanzibar.

**<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>**

64. MHESHIMIWA JABU MAKAME JUMA (Nafasi za Wanawake) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Wakati wa ufunguzi wa Skuli ya Tumbatu, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, aliahidi kuimarishwa Ofisi za Serikali ili kuifanya Tumbatu kuwa Wilaya kamili. Katika hali tuliyonayo hivi sasa, wananchi wa Tumbatu wananufaika na Hospitali ya Wilaya, Skuli ya Wilaya na Ofisi Ndogo ya Wilaya, lakini bado haijawa Wilaya kamili kama ilivyoahidiwa.

(a) Je, ahadi ya kuitangaza Tumbatu kuwa Wilaya kamili imekwama wapi.

(b) Ni lini ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ya kuifanya Tumbatu kuwa Wilaya kamili itatimizwa.

**Wizara ya Fedha na Mipango:**

204. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Kumekuwa na mtindo wa baadhi ya taasisi za Serikali zinazokusanya mapato kutoa adhabu ya faini kwa walipa kodi kwa kuchelewa kulipa kwa wakati kwa sababu mbalimbali. Hatua hii imekuwa ikiwavunja moyo walipa kodi na wawekezaji kwa vile wakati mwengine wanakuwa na sababu za msingi za kuchelewa huko.

Je, Serikali itachukua hatua gani kuondosha changamoto hiyo na kuweka mazingira rafiki ya walipa kodi.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

46. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa somo la Saikolojia linafundishwa mashuleni kwa lengo la kuwanusuru watoto wetu na athari za kulikosa somo hili.

103. MHESHIMIWA MOHAMMED ALI SALIM (Jimbo la Ziwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa Ualimu ni moja kati ya kazi ngumu sana inayohitaji takwimu za utulivu wa hali ya juu ukilinganisha na kazi nyengine. Na kwa kuwa katika Utumishi wa Umma, mbali na mishahara ya kila mwezi kuna stahiki nyengine wanazopewa watumishi kwa lengo la kujenga hamasa katika utumishi wao, ikiwemo posho maalum kwa ajili ya likizo la mwaka.

(a) Je, sababu gani za msingi zinazopelekea walimu katika nchi hii kucheleweshewa au kutolipwa posho hiyo kwa kipindi kirefu.

(b) Kwa kuwa kuwanyima Walimu wa Msingi na Sekondari posho maalum ya likizo ya mwaka ni kuwavunja moyo na kurudisha nyuma sekta ya elimu nchini, je, Serikali inatoa kauli gani juu ya suala hili.

**Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:**

164. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

Serikali imewekeza rasilimali kubwa za umma katika ujenzi wa viwanja vikubwa vya michezo vinavyokidhi viwango vya kimataifa (International Standards), kwa lengo la kukuza vipaji vya vijana, kuendeleza sekta ya michezo na kuinua taswira ya taifa katika mashindano ya kikanda na kimataifa.

Katika kutekeleza dhamira hiyo njema, Serikali imechukua hatua ya kuvikodisha baadhi ya viwanja hivyo, ili kuhakikisha vinatumika kikamilifu, vinajiendesha kibiashara na vinachangia katika kurejesha gharama za uendeshaji na matengenezo.

(a) Je, Serikali ina mpango gani mahsusi wa usimamizi, matumizi na uendelezaji wa viwanja vyengine vilivyobakia.

(b) Je, Serikali inawahakikishia vipi wananchi, hususan vijana na vilabu vya michezo, kuweza kuvitumia viwanja vilivyojengwa na kukodishwa, kwa lengo la kukuza michezo hapa nchini.

(c) Kwa kuwa viwanja hivyo vimekodishwa, je, Serikali inatoa vipi bei elekezi za viingilio na miongozo ya matumizi ya viwanja hivyo, ili manufaa yake yawafikie moja kwa moja wananchi wetu.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

89. MHESHIMIWA ALLEY MASOUD ALLEY (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Kwa kuwa kila mwaka Serikali inajipatia kipato kwa kulikodisha Diko la Likoni lililopo Kengeja kwa gharama kubwa.

Je, ni lini eneo la Diko la Likoni litajengwa la kisasa linaloendana na kasi ya maendeleo mapya wanayoyahitaji wananchi wetu.

**Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji:**

133. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Ajira na Uwezeshaji:

Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi ikiwemo Mifuko ya Inuka, *Khalifa Fund* na Mikopo ya Makundi Maalum (4:4:2). Pamoja na utoaji huu wa fedha kumekuwa na changamoto ya urejeshaji wa fedha hizi ambazo ni za walipa kodi.

(a) Je, ni ipi tathmini ya urejeshaji wa fedha katika mifuko hii kiwilaya.

(b) Je, ni taasisi gani za Serikali na Serikali za Mitaa ambazo hushindwa kuwasilisha mikopo kwa mujibu wa mkataba, ikiwemo asilimia 10 ya mkopo wa 4:4:2

**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:**

75. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Kwa kuwa Serikali inatoa ahadi ya ujenzi wa barabara ya Vitongoji Kibokoni mara kwa mara. Na kwa kuwa wananchi wa maeneo hayo hawaoni juhudi zozote za utekelezaji wa ahadi hiyo.

Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuitimiza ahadi yake hii.

128. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Kumekuwa na malalamiko makubwa ya wafanyabiashara wanaoingiza mizigo yao, ikiwa ni pamoja na makontena kutokea nje ya nchi kupitia bandari ya Zanzibar, kwa mteja kutakiwa kulipia gharama ya kulisafirisha kontena kwa wastani wa Shilingi za Kitanzania 600,000/- kutoka bandarini hadi bandari kavu ya Maruhubi.

(a) Kwa kiasi kipi Serikali inalitambua tatizo hili linalowakumba wafanyabiashara.

(b) Kwanini gharama za kulisafirisha kontena kwenda Maruhubi zinalipwa na mteja badala ya kulipwa na muwekezaji husika.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

177. MHESHIMIWA SAID AZANA MSINGIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Wananchi wengi wa jimbo la Uzini wanategemea kilimo katika kuendesha maisha yao. Hata hivyo, kutokana na hali zao za kimaisha wanaendelea kulima kwa kutumia zana za kizamani ambazo haziwapi mafanikio makubwa katika kulima huko.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha wananchi wa jimbo la Uzini, ili walime kilimo cha kisasa.

(b) Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kuwa wananchi hawa wanakuwa na uelewa mpana wa kilimo cha kisasa.

**Wizara ya Afya:**

4. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Je, Serikali imefikia wapi katika kupunguza vifo vya mama na mtoto wakati wa kujifungua.

94. MHESHIMIWA MOHAMMED ALI SALIM (Jimbo la Ziwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Pamoja na uwepo wa majengo mazuri ya hospitali ya Wilaya ya Chake Chake iliyopo Vitongoji, kuna usumbufu mkubwa wa wagonjwa kupata huduma ya matibabu. Wagonjwa hutumia

muda mrefu na kuna msongamano mkubwa katika taratibu za foleni kwa ajili ya kupata matibabu hospitalini hapo.

Je, kitu gani kinachopelekea kuwepo usumbufu wa kupata huduma za matibabu katika hospitali hiyo.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

1. MHESHIMIWA MARIAM SAID KHAMIS (Nafasi za Wanawake) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

   Serikali inaendelea kuboresha huduma ya maji safi na salama katika maeneo ya mjini na vijijini.

   Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha huduma ya maji safi na salama katika jimbo la Mkoani.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

51. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

    Vitendo vya ukatili na udhalilishaji vinaendelea kushuhudiwa nchini siku hadi siku, pamoja na mikakati na jitihada zinazochukuliwa na Serikali yetu ya kuvipunguza na hatimae kuviondosha kabisa.

    Je, kuna mpango gani wa ziada wa kupambana na tatizo hilo.

## II. TAARIFA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Fedha na Mipango:**

Taarifa ya Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2026/2027.

**Zanzibar,**
**18 Februari, 2026.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA**
**WAWAKILISHI, ZANZIBAR**